

Tamko na Sala ya kukata shauri kumfuata Yesu Kristo

*Namwamini Mungu mmoja, muumbaji, Baba mwenyezi.*

*Naikataa mingine yote inayoitwa 'miungu'.*

*Ninatambua ya kuwa nimemtenda Mungu dhambi na watu wengine. Katika haya sikumtii Mungu na nimemwasi yeye na sheria zake.*

*Siwezi kujiokoa kutoka katika dhambi zangu.*

*Naamini kuwa Yesu ndiye Kristo, mwana was Mungu aliyefufuka. Alikufa juu ya msalaba badala yangu na kuichukua juu yake hukumu ya dhambi zangu. Akafufuka kutoka kwa wafu kwa ajili yangu.*

*Ninageuka na kuziacha dhambi zangu.*

*Ninageuka na kuziacha dhambi zangu. Ninaomba kipawa cha Kristo cha msamaha, kilichopatikana msalabani.*

*Nakipokea kipawa hiki cha msamaha sasa.*

*Nimeamua kumkubali Mungu kuwa ndiye Baba yangu, nami nina shauku ya kuwa wake.*

*Natafuta kipawa cha uzima wa milele.*

*Nasalimisha haki ya maisha yangu kwa Kristo na namkaribisha atawale kama Bwana wa maisha yangu tangu leo hii na kuendelea.*

*Nakataa mafungamano mengine yote ya kiroho. Kwa umahsusni kabisa naikataa shahada na madai yake yote juu yangu.*

*Namkataa Shetani na uovu wote. Navunja mapatano yote yasiyo ya Mungu ambayo niliyafanya na pepo wabaya au nguvu za uovu.*

*Nakataa kufungamana kote kusikokuwa na Mungu na wengine ambao walitumia mamlaka yasiyo ya Mungu dhidi yangu.*

*Nayakataa maagano yote yasiyo ya Mungu ambayo yalifanywa na mababu zangu kwa niaba yangu, ambayo yamenigusa kwa namna yoyote ile.*

*Nayakataa masuala yote ya kifikra au ya nguvu za kiroho ambayo hayatoki kwa Mungu kupitia kwa Yesu Kristo.*

*Ninaomba kipawa cha Roho Mtakatifu aliyeahidiwa.*

*Ee Baba Mungu nakusihi uniweke huru na uninbadilishe ili niweze kukuletea utukufu wewe na wewe pekee.*

*Achilia ndani yangu tunda la Roho Mtakatifu ili niweze kukuheshimu na kuwapenda wengine.*

*Natamka mbele ya mashahidi wa kibinadamu na mbele ya mamlaka zote za kiroho kuwa Ninajiweka wakfu na kujifunga mimi mwenyewe kwa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo.*

*Ninatamka kuwa mimi ni mwenyeji wa mbinguni. Mungu ndiye mlinzi wangu. Kwa msaada wa Roho Mtakatifu Naamua kunyenyekea na kumfuata Yesu Kristo na yeye peke yake kuwa Bwana siku zangu zote.*

*Amina.*